

# Ving'ora vya Moshi Huokoa Maisha




Ving'ora vya moshi vinavyofanya kazi huokoa maisha.

*Kila nyumba huko Massachusetts lazima iwe na ving'ora vinavyofanya kazi vya moshi.*

## Huenda ukawa na chini ya dakika tatu kuepuka moto nyumbani.

- Ving'ora vya moshi vinavyofanya kazi hukutahadharisha kuhusu hatari. Vinaweza kukupa muda wa kuondoka kwenye jengo kabla ya moshi mbaya, na miali ya moto na gesi zenye sumu kuzuia njia yako ya kuponyoka.
- Kuwa na ving'ora vya moshi vinavyofanya kazi ndani ya nyumba yako kunaweza kuongeza uwezekano wako wa kuishi ikiwa moto utawaka.
- Vifo vya moto majumbani vimepungua kwa nusu tangu mwanzoni mwa miaka ya 1970 wakati ving'ora vya moshi vililipouzwa kwa mara ya kwanza.

## Badilisha saa yako / Kagua ving'ora vyako.



**Ikiwa ving'ora vimetumika zaidi ya miaka 10, vibadilishe sasa.**

## Ving'ora vya moshi haviwezi kukusaidia ikiwa havipatikani au havifanyi kazi.

- Cha kusikitisha, zaidi ya watu 3,000 bado wanakufa kwa moto kila mwaka nchini Marekani.
- Takriban 60% ya vifo vya moto nyumbani hufanyika katika nyumba zisizo na ving'ora vya moshi.

## Kuwa salama, kuwa mwangalifu, ulindwe.

- Weka ving'ora vya moshi kwenye kila sehemu ya nyumba yako, ikiwemo sehemu ya nyumba iliyo chini ya ardhi.
- Vipime kila mwezi.
- Badilisha betri za alikali mara mbili kwa mwaka wakati unabadilisha saa zako.
- Badilisha king'ora baada ya miaka 10.
- Usiwahi kuzima king'ora au kuondoa betri kwa sababu yoyote.

## King'ora kinapoita:

- Wafundishe watoto wako na familia kuondoka kwenye jengo mara moja wanaposikia king'ora cha moshi.
- Toka nje na ukae nje.



Department of Fire Services  
www.mass.gov/dfs • (978) 567-3100




- Nenda kwenye mahali pa kukutana na familia.
- Piga simu kwa 9-1-1 ukiwa nje au katika nyumba ya jirani.

**Ving'ora maalum vya moshi vinapatikana kwa watu ambao ni Viziwi au wenye ugumu wa kusikia.**

King'ora cha mtetemo kinaweza pia kutumika chini ya mto mtu akiwa amelala. Fikiria kifaa kilicho kando ya kitanda ambacho huhisi sauti ya ving'ora vya moshi.

**Panga njia na ufanye mazoezi ya kutoroka moto nyumbani.**

- Panga njia mbili za kutoka kwenye jengo lako na njia mbili kutoka kwa kila chumba, ikiwa inawezekana.
- Jadili mpango huu ili kila mtu katika familia yako aelewe anachopaswa kufanya ikiwa hali ya dharura itatokea.
- Chagua mahali nje ya nyumba ambapo wanafamilia wanaweza kukutana ili kuhakikisha kuwa kila mtu yuko nje ya jengo salama.
- Watoto wadogo, wazee, na watu wenye ulemavu wanaweza kuhitaji usaidizi wa ziada.



**Miongozo ya jumla ya kuweka king'ora cha moshi**

- Kwenye kila sehemu ya nyumba yako.
- Katika barabara za kupita nje ya chumba cha kulala.
- Katika sehemu ya juu ya ngazi zilizo wazi.
- Chini ya ngazi za sela.

# Kagua ving'ora vya moshi kila mwezi.

- Ndani ya chumba cha kulala kwa watu wenye usingizi mzito au wavuta sigara.
- Wasiliana na idara ya zima moto iliyo karibu nawe ili upate maeneo hususa.

**Matengenezo.**

- Mara moja kwa mwezi, toa vumbi kutoka kwenye king'ora.
- Bonyeza kitufe cha jaribio.
- Iwapo kengele inatumia betri za kawaida, zibadilisha mara mbili kwa mwaka unapobadilisha saa zako. Sauti "nyembamba" inamaanisha kuwa ni wakati wa kubadilisha betri.
- Usipake rangi ving'ora vya moshi.

**Badilisha Ving'ora vya Moshi Baada ya Miaka 10**

- Angalia tarehe ya utengenezaji iliyochapishwa kwenye sehemu ya nyuma ya ving'ora vyako. Ikiwa kengele imetumika zaidi ya miaka 10, ibadilisha mara moja.
- Unaponunua king'ora kipya cha moshi, chagua kilichofungwa, betri ya kudumu na kifaa chenye kipengele cha kunyamazisha. Chagua king'ora kutoka chapa maarufu inayojulikana kitaifa.
- Iwapo unatatizika kununua, kuweka au kutengeneza ving'ora vya moshi, piga simu kwa idara ya zimamoto iliyo karibu nawe.